# Akisiko la Hali na Mtazamo Hasi wa Maendeleo ya Mwanamke katika Jamii: Mifano Kutoka katika Riwaya ya *Wasifu wa Siti Binti Saad*

**By**

**Hadija Rashid Utukulu & Omary Mohamed Maguo**

Chuo Kikuu Huria cha Tanzania
hadijautukulu2@gmail.com

**Ikisiri**
Makala haya yamechunguza hali na mtazamo hasi wa maendeleo ya mwanamke katika jamii kwa kurejelea riwaya ya Kiswahili.Data za msingi zimepatikana katika riwaya ya *Wasifu wa Siti Binti Saad* kwa mbinu ya usomaji makini. Mapitio ya nyaraka zilizotumika kufafanua data za msingi zilipatikana kwa mbinu za kieletroniki na kimaktaba.Uchambuzi na mjadala wa data zilizowasilishwa uliongozwa na nadharia ya Ufeministi.Makala haya yanaelezea namna mwanamke anavyoakisiwa katika shughuli mbalimbali za kijamii kupitia utanzu wariwaya ya Kiswahili. Aidha, inadokeza hali halisi ya maisha na matokeo ya harakati za mwanamke pamoja na namna jamii inavyomtazama katika maisha yake ya kila siku. Makala haya yanalenga kuchochea mwamko thabiti wa fikira zake ili kunyanyua na kutetea nafasi, hadhi na thamani ya kiutu anayostahiki katika ngazi na asasi mbalimbali za kijamii. Makala hii inahitimisha kuwa mwanamke hapaswi kutazamwa katika hali ya kupuuzwa na kukandamizwa badala ya kumtazama kama mhimili thabiti katika mifumo ya malezi, uzalishaji mali na uchumi katika ngazi zote za jamii na taifa.

**Maneno Msingi:** Hali, Hadhi, Mtazamo Hasi, Mwanamke na Fasihi ya Kiswahili,

## 1.0 Utangulizi

Fasihi ya Kiswahili iimejengwa katika uwanja mpana unaohakiki hali na harakati za maisha ya kila siku ya jamii hapa nchini na kwingineko barani Afrika. Kupitia utanzu huo, suala la maisha ya binadamu limejadiliwa kwamielekeo na maoni tofauti. Maisha ya binadamu yamechunguzwa katika ngazi zote za maisha yake tangu uzazi, malezi, ndoa, uzee hadi kifo (Fakih, 2017). Kila ngazi katika maisha ya binadamu ina harakati zake. Hali hiyo inatokana na kwamba kila jamii ina vikwazo vyake, miiko yake na masharti yake yanayomwongoza binadamu. Kanuni za jamii humfunga binadamuna kuingilia matakwa na shughuli zake za kujiendeleza kimaisha na kimtazamo. Katika harakati hizo, binadamu wana matatizo yao, matakwa yao na maslahi yao yanayojidhihirisha katika kazi za fasihi.

Historia ya kudunishwa kwa mwanamke katika jamii za ulimwengu ni ndefu kwani inarudi nyuma hadi enzi zile jamii ya watu ilipoanza kugawanyika katika matabaka. Katika baadhi ya jamii kulikuwa na vipindi vya kihistoria ambamo wanawake walitawala kiuchumi na kisiasa

(Mapunjo, 2014). Hali hii ilitokea jamii ilipoanza kugawanyika na kutokea wale waliomiliki njia za uzalishaji mali na uchumi; ndipo mwanaume alipoanza kuwakilisha nguvu za uchumi na kuzitumia nguvu hizo kufanya lolote dhidi ya mwanamke. Uhusiano huo ulizidi kukuzwa na taasisi mbalimbali za kijamii, hasa za kidini na kindoa zilizoambatana na utoaji wa mahari. Suala la mahari linatazamwa katika misingi ya kumnunua mwanamke hali inayoendelea kumpa mwanaume wigo mpana wa kumtumia kwa namna anavyotaka.

Hali ya kupuuzwa kwa mwanamke katika jamii imefungamana na mkabala wa mwanamke kutumiwa kama chombo cha duni cha uzalishaji mali na kuendeleza kizazi katika jamii ya mwanadamu. Hali hii inatokana na sababu za kiutamaduni na fikra potofu zilizoshamira katika jamii kuhusu hali na hadhi ya mwanamke katika jamii (Githuci, 2013). Utatuzi wa mgogoro huo una mikabala mingi kufuatana na mitazamo ya jamii. Aidha, suala la usawa na ukombozi wa mwanamke halina misingi imara ya kiutamaduni, kiuchumi na kisiasa; na uduni wake unajitokeza wazi wazi katika asasi mbalimbali za kijamii. Wanaume wanaendelea kuwasilisha nguvu za kiuchumi na kimadaraka katika asasi mbalimbali za kijamii na kitaifa.

Hali ya wanaume kuendelea kuwasilisha nguvu za kiutamaduni na kiuchumi imewafanya wanazuoni wengi kuichunguza nafasi ya mwanamke kupitia kazi za fasihi. Kwa mfano, Massoud (2018) anaeleza kuwa suala la ujinsia halijashughulikiwa vya kutosha katika uhakiki wa kifasihi, hasa katika fasihi za Kiafrika, ikiwamo fasihi ya Kiswahili. Wahakiki wengi wa fasihi za Kiafrika wanakumbana na wanawake katika miktadha mbalimbali, lakini wanakwepa kuchunguza na kuhakiki uhusika wao katika fasihi ya Kiswahili kutokana na kuwepo kwa sababu mbalimbali. Wasanii wengi wanamchora mwanamke katika sura mbalimbali kulingana namielekeo na maoni tofauti katika fasihi ya Kiswahili.

Baadhi ya wataalamu wamemtazama mwanamke kama mfungwa anayewekwa ndani muda wote pasipo kupewa ruhusa ya kutoka nje. Hali hiyo inamfanya mwanamke kunyimwa haki zake za msingi, pamoja na uhuru wa kutembea kutoka eneo moja kwenda eneo jingine. Jambo hilo lilimfanya Ruto (2015) kuzishambulia na kuzikosoa baadhi ya asasi zinazochangia kuendelea kumdhalilisha na kumdunisha mwanamke katika jamii. Suala la kudhalilishwa na kudunishwa kwa mwanamke linapatilizwa na Sungi (2011) anapoeleza kuwa kuna mtazamo potofu ulioanzishwa na asasi za kijamii za kumwona mwanamke kama chanzo cha uovu katika jami bila kuchunguza kwa kina mchango wa mwanaume katika kumfanya mwanamke aoneshe tabia zisizofaa. Hali hii inasababishwa na kutamalaki kwa mifumo ya utamaduni inayomtaka mwanamke awe mnyenyekevu na mtiifu kwa mumewe.

Wapo waandishi wanaosisitiza kuwepo kwa usawa kati ya mwanaume na mwanamke katika jamii. Hali hiyo huwafanya wanawake wengi kupata nguvu na sauti katika maeneo mengi jambo linalosababisha kujengwa kwa jamii inayoanza kuweka misingi ya usawa na haki katika jamii

nyingi hapa nchini na kwingineko barani Afrika. Hali hiyo ilimfanya Lyatuu(2011) kueleza kwamba wanawake lazima wasimame kidete kwa nguvu zao ili wajitetee na kupambana kwa dhati kwa sauti zao wenyewe na kuacha kuwategemea wanaume ambao kimsingi ndiyo wanaodhulumu haki wanazopigania. Wanawake hawana budi kupigania haki zao katika taifa lao ili kuhakikisha kuwa elimu, kazi, afya na huduma za kiuchumi zinatolewa kwa usawa. Kupigania haki zao ni pamoja na kuhakikisha kuwa wanawake wanashiriki katika nafasi mbalimbali za uongozi katika maeneo ya ngazi za maamuzi pasipo kubaguliwa.

Wahakiki na watafiti wengi wamejaribu kwa kiasi fulani kushughulikia suala la mwanamke kwa namna mbalimbali. Wengi wanaelekea kuafiki kuwa miundo ya kijamii pamoja na asasi zake inaashirikiana kumkandamiza mwanamke. Suala la utamaduni linatazamwa kama mhimiri mkuu unaosababisha kumdunisha mwanamke katika jamii (UN, 2014). Mifumo ya kiutamaduni iliyopo katika jamii imechangia kumchora mwanamke katika mitazamo chanya na hasi. Huu ndio msingi wa makala hii iliyolenga kuchunguza hali na mtazamo hasi wa maendeleo ya mwanamke katika jamii kwa kurejelea riwaya ya Kiswahili.

## 2.0 Mbinu na Nadharia ya Utafiti

Makala haya yamechunguza hali na mtazamo hasi wa maendeleo ya mwanamke katika jamii kwa kurejelea riwaya ya Kiswahili. Data za msingi zimepatikana katika riwaya ya *Wasifu wa Siti Binti Saad* kwa mbinu ya usomaji makini. Mapitio ya nyaraka zilizotumika kufafanua data za msingi zilipatikana kwa mbinu za kieletroniki na kimaktaba.Uchambuzi na mjadala wa data zilizowasilishwa uliongozwa na nadharia ya Ufeministi.Mtazamo wa Ufeministi una historia ndefu duniani kwa kuwa uliibua vuguvugu la kutaka kufuta kabisa suala la uonevu dhidi ya mwanamke. Agenda ya Ufeministi inalenga kumaliza utawala wa mwanaume dhidi ya mwanamke. Ili kufanikiwa, wanawake wanahitaji kubomoa kabisa miundo ya mihimili ya utamaduni wa jamii iliojengeka katika sanaa, dini, sheria na kaya zinazodhibitiwa na mfumo wa kibaba na taswira zote za asasi zinazomwona mwanamke kama mtu dhaifu.

Katika makala hii, riwaya teule zilichunguza namna sura ya mwanamke inavyoaminika na kukubalika katika jamii ya wakati wake. Nafasi ya mwanamke ilichambuliwa na kuhakikiwa kulingana na uhusiano wa moja kwa moja uliopo kati ya jamii na hali halisi iliyopo katika jamii za Tanzania. Hali hii ni kwa sababu kazi ya fasihi inadhibitiwa na miundo iliyopo katika jamii kwa kuzingatia uhusiano wa wanajamii katika mienendo yao ya maisha yao ya kila siku. Riwaya teule itachunguzwa kama zao mahususi la jamii hiyo kwa kuzingatia historia yao, falsafa zao, mila na desturi zao, uchumi na siasa zao; na zilichunguzwa kama kiungo maalumu cha mahusiano ya kijamii.Nadharia hii imetumika kuchunguza hali, hadhi na maendeleo hasi ya mwanamke yanavyoakisiwa katika fasihi ya Kiswahili.

## 3.0 Mtazamo Hasi wa Mwanamke Unavyoakisiwa katika Riwaya Teule

Makala haya yamechunguza hali, hadhi na maendeleo hasi ya mwanamke yanavyoakisiwa katika fasihi ya Kiswahili. Uchunguzi umeonesha namna mwanamke anavyotazamwa katika katika jamii kwa kujikita katika riwaya teule. Katika riwaya teule suala la nafasi hasi ya mwanamke inavyoakisiwa limechunguzwa katika sura mbalimbali kama ilivyoelezwa katika sehemu inayofuata.

**3.1 Haki ya Kushiriki katika Shughuli za Uzalishaji Malina Uchumi**

Katika baadhi ya jamii, inaaminika kuwa shughuli za uzalishaji mali na uchumi ni jukuu la mwanaume pekee na si mwanamke. Jambo hilo linasababisha kuzorota kwa maendeleo ya mwanamke, familia na taifa kwa ujumla kwa kuwa mwanamke ni mzalishaji mkuu katika jamii nyingi barani Afrika. Hali inamfanya mwanamke awe tegemezi katika masuala mbalimbali ya usimamizi wa familia na maisha yake mwenyewe. Kuendelea kufanya hivyo ni kuendelea kumnyima fursa pana ya kushirika katika maendeleo ya jamii na taifa lake. Mbiu (2013) anasisitiza kuwa jamii inapaswa kutambua kuwa suala la uzalishaji mali na uchumi halipaswi kuegemezwa upande mmoja tu mwanaume na kumwacha mwanamke nyuma kabisa ili kuyafikia maendeleo na kujenga jamii endelevu. Mwandishi anaeleza:

> Inasemwa mara kwa mara kwamba katika maisha mwanamke alikuwa na mapigano mengi kama mwanaume. Kama hili lilikuwa si mzaha wa kupitisha wakati, basi ilikuwa wajibu wa kila nchi kuandaa wanawake wote kwa mapigano yao. Kufaulu kwao kulikuwa kushindwa kwa watu wote. Umati wa wanawake wa kazi na matendo mbalimbali kama Siti alivyokuwa ndilo jeshi lililotakiwa katika wokovu wa maisha katika Afrika Mashariki (Uk. 58),

Ufafanuzi huo unasisitiza kuwa suala la uzalishaji mali na uchumi katika jamii ni umhimu kufanywa na kuwa katika mikono ya mwanamke na mwanaume ili kuleta maendeleo ya haraka ya kiuchumi katika jamii. Ushirikiano wa pande mbili utajenga umoja thabiti wa kufanya kazi kwa manufaa ya kuendeleza familia na taifa lao. Umoja ni fimbo ya mnyonge. Suala la umoja na bidii katika uwajibikaji ni miongoni mwa mambo ya msingi katika kuinua uchumi wa familia, jamii na taifa. Uwajibikaji ni nyenzo muhimu katika kuyamudu mahitaji ya msingi (Mabuba, 2015). Pia, huiasa jamii kufanya kazi kwa umoja, mshikamano na bidii. Umoja ni fimbo ya mnyonge katika jamii na taifa lolote. Umoja na shina la maendeleo, na ni silaha bora dhidi ya umaskini.

Katika mfumo wa biashara nchini, wanawake hawapati mikopo kwa urahisi kama jitihada mojawapo ya kumudu harakati zao za kibiashara. Wengi wao hawana uwezo wa kuendesha biashara zao katika kiwango kinachofaa kutokana na kukosekana kwa mitaji inayokidhi harakati zao za msingi (Sanga, 2013). Pia, wanawake hawakopesheki na hawaaminiki katika taasisi zinazojihusisha na masuala ya fedha kutokana na kuwapo kwa sababu mbalimbali. Wengi

hawafanyi biashara zao kisasa kutokana na ukosefu wa mitaji yenye tija. Pengo linalobainishwa huwafanya wanawake walio wengi kutokuwa na sauti katika maeneo mengi.

Aidha, ipo haja ya kujenga vyombo na taratibu zitakazojali nafasi za maumbile katika shughuli za maendeleo. Miundo ya mikakati, mitazamo ya ushirikishaji wa kiwakati na kisera, mafunzo ya mawakala wa maendeleo na marekebisho ya taratibu za uendeshaji na za sheria, lazima vyote vioneshe jukumu muhimu walilonalo wanawake katika kujenga uchumi wa jamii na taifa, hasa katika shughuli za uzalishaji mali na uchumi katika ngazi zote za kijamii.Fikira hizo zinahitajika kubadilika katika jamii zote, hasa katika jamii ambazo hisia za mwanamke kuwa duni kuliko mwanaume zinaendelea kutamalaki, na ambako hirizi ya utamaduni mbovu unaoendelea kutumiwa kuhalalisha kubaguliwa kwao (Maganga, 2016). Kwa kutambua majukumu ya maendeleo ya taifa, lazima wanawake washirikishwe na kuwezeshwa kikamilifu katika shughuli zote za maendeleo ya jamii na taifa.

**3.2 Haki ya Kujishughulisha naSanaana Muziki**

Kutokana na kuwepo kwa imani potofu zilizoshamiri katika baadhi ya jamii hapa nchini na kwingineko barani Afrika, mwanamke hakuruhusiwa kujishughulisha na masuala yanayohusiana na sanaa. Mwanamke alidiriki kufanya hivyo alitazamwa kama malaya. Jambo hilo lilisababisha kuwanyima wanawake kushiriki kikamilifu katika masuala ya kiutamaduni na hata kudumaza vipaji vyao na kukosa kipato cha kujikimu kwa sababu sanaa ni sehemu ya ajira. Hali ya kumchukulia mwanamke kama malaya akishiriki katika masuala ya sanaa na utamaduni katika jamii yake, lilimfanya Kitundu (2012) atoe kauli ya kuacha tabia kumpuuza mwanamke na kumdhalilisha kiutamaduni. Pia, alionesha kuwa bado mwanamke anapewa nafasi duni inayomdhalilisha mwanamke kama chombo cha starehe, malaya, mchawi ama kiumbe dhaifu. Katika riwaya teule mwandishi anaonesha namna Siti alivyokuwa na kipaji cha sauti, lakini hakujua jinsi ya kukitumia vema kutokana na kuwepo kwa imani potofu katika jamii yao. Mwandishi anaeleza:

> Siti alikuwa na kipawa cha sauti, lakini alikuwa hajui jinsi ya kukikuza wala kukipalilia. Pia, hakujua jinsi ya kushika pahali pake katika tamasha. Alikuwa hana msingi wowote wa kujengea kuta za ustawi wake (Uk. 11).

Maelezo haya yanaonesha kuwa wanawake wengi katika jamii za Kiafrika wana vipaji vya uimbaji katika tasinia ya muziki na sanaa, lakini hawapewi nafasi kutokana na kuwepo na kushamiri kwa imani potofu zinazomtazama mwanamke mwanamuziki ni mhuni, malaya na hawezi kumudu harakati za malezi ya familia yake. Jamii inapaswa kuelewa kuwa mwanamke anahitaji kupata fursa pana ya kujiendeleza kiuchumi na kijamii kwa kujiari kupitia fani ya muziki na sanaa. Hoja hii inapewa uzito na Omary (2009) anayesisitiza kuwa sanaa ya muziki ni sehemu ya ajira kwa wasanii na wadau wengine wanaojihusisha na kazi za kisanaa. Mtazamo

huo umo katika muziki wa kizazi kipya, ambapo vijana hujiingiza katika mkondo huo ili kujipatia riziki. Vijana hujiingiza katika muziki wa bongo fleva au kizazi kipya kwa madhumuni tofauti tofauti yakiwamo ya kujipatia ajira.

### 3.3 Kubaguliwa katika Shughuli za Kijamii

Kwa kawaida, hakuna shughuli isiyohitaji umoja na ushirikiano katika jamii ya Tanzania na kwingineko barani Afrika. Ushirikiano hutazamwa kama mbinu mojawapo ya kuunganisha nguvu katika harakati mbalimbali za jamii hiyo. Pia, hutazamwa kama nguzo imara inayosaidia kufanikisha harakati za maendeleo ya jamii na taifa (Challigha, 2011). Umoja huleta tija na ufanisi katika shughuli zote za kijamii. Suala hilo limepewa nafasi kubwa na wasanii wa fasihi ya Kiswahili kwa kusisitiza suala la kufanya kazi kwa ushirikiano ili kupata ufanisi katika kila fani ya maendeleo. Umoja hutazamwa kama fimbo ya mnyonge katika harakati za kukabiliana na shughuli za kila siku.

Umoja ni chachu ya mafanikio katika shughuli zote za kijamii. Jamii za Kitanzania hazina budi kujenga misingi imara ya kushirikiana ili kuyabili mazingira yao kwa kadiri zitakavyoweza. Huu ndio msingi unaoipa jamii fursa pana kumchukulia hatua na kutoa adhabu kali kwa yeyote asiyeshiriki kikamilifu katika shughuli za kijamii. Hata hivyo, katika baadhi ya jamii hapa nchini, bado zinamtazama mwanamke kama hastahili kufungamana na mwanaume katika shughuli za uchumi, siasa, sanaa na hata dini. Haja yao inaangukia kumchora mwanamke kama hana mchango wowote wenye kulete tija na maendeleo katika kujikomboa katika nyanja zote za kijamii.Oyoronke (2005) anaeleza kuwa katika baadhi ya jamii za Kiafrika, mwanamke haruhusiwi kusimama mbele ya mkutano wa wanaume, labda kama ana kesi ya kujibu. Jamii ikiendelea kufanya hivyo itachelewa kuyafikia maendeleo chanya yanayohitaji nguvu moja inayotokana na jinsia zote mbili zisizobaguana.Mwandishi anaonesha Siti alivyokuwa akipewa nafasi finyu akiwa katika jumuiya ya muziki, licha ya kuwa umaarufu wake uliotokana na uimbaji wa kutegemewa. Mwandishi anaeleza:

> Baadaye, Siti alijiunga na Jumuiya ya Watribu maarufu sana wakati ule, Subri Ambari (mpiga udi), Buda Swedi (mpiga gambusi), mwalimu Shabaani (mpiga tari ya Mbaruku), katikati ya wanaume watoto, mwanamke alikuwa mmoja tu, yaani, Siti. Ndiye alikuwa mwimbaji peke yake kati ya vinanda vyao (Uk. 12).

Maelezo haya yanaonesha kuwa baadhi ya jamii hazikuona fahari ya mwanamke kuchangamana na wanawake, isipokuwa katika baadhi ya mambo ambayo mwanaume hakuwa na uwezo wa kuyafanya. Kwa mfano, katika nukuu hiyo, Siti alikuwa mwanamke pekee aliyetegemewa kwa upande wa uimbaji. Upekee wa Siti na uwezo wake wa uimbaji unaifanya jamii isimchukulie mwanamke kama mtu asiye na uwezo wa kushiriki kwa dhati katika shughuli za kijamii. Pengo

la nafasi ya uimbaji lilizibwa na Siti katika jumuiya aliyokuwa amejiunga, licha ya kuwa ilikuwa na wanaume wengi. Hoja hii inaonesha kuwepo kwa hali na haja ya kutegemeana na kuchukuliana katika jitihada za kuyakabili maisha, utamaduni na mazingira. Wanawake wameendelea kuachwa nyuma katika masuala ya msingi ya kimaendeleo pamoja na yale yanayohusu suala la siasa, utamaduni na uchumi bila sababu za msingi.

Kwa upande mwingine, katika baadhi ya jamii wanawake wanabaguliwa kutokana na kuwepo kwa mgawanyo usio sawa wa kimamlaka kati ya wanaume na wanawake katika nyanja mbalimbali za kijamii; na wanaoonekana kama watu wa kuongozwa tu. Matokeo yake, uwezo wa wanawake kiuongozi umenyamazishwa bila sababu za msingi (Khatibu, 2011). Jambo hili linatokana na mfumo wa jamii unaoamini kuwa mwanamke hawezi kuwa kiongozi imara kama wanaume walivyo. Tofauti na mtazamo huo, mwandishi anaonesha namna Siti alivyosaidia jumuiya aliyojiunga kuinuka kwa upande wa hadhi na kipato maridhawa. Jamii isichukulie kuwa kila jambo lenye tija litafanywa na mwanaume tu. Mwandishi anaeleza:

> Yeye alikuwa mwanamke wa kwanza katika kisiwa cha Unguja aliyejiunga katika kazi ile ya starehe.Subeti, Buda, Shabaan na Mbaruku walikuwa wakipata fedha kidogo, kwanza walianza kulipwa fedha maridhawa sana (Uk. 12).

Ufafanuzi huu unaonesha kuwa jamii ikimpa mwanamke kipaumbele cha kuaminiwa na kupewa majukumu anaweza kusaidia sana kuleta maendeleo chanya katika jamii. Mwanamke ana uwezo wa kubadilisha mtazamo hasi na kuwa chanya kulingana na namna anavyofikiri, anavyofanya kazi kwa bidii, kujituma na kwa uzalendo wa hali juu (Bond, 2000). Pia, mwanamke ni kichocheo cha maendeleo katika nyanja mbalimbali za maisha, kiutamaduni na kimazingira. Hakuna asiyefahamu kuwa mwanamke ni nguzo kuu katika uzalishaji mali na kukuza uchumi wa familia, jamii na taifa (Pullen, 2006). Sera ya kulinda na kuhimiza uwezo wa wanawake wa kushiriki kuinua mchango wao katika sekta zote za uchumi na kuimarisha jinsi ya kujitegemea, ushirikishwaji wa umma, pamoja na kulinda mazingira linapaswa kuchunguzwa upya kwa manufaa endelevu ya jamii na taifa. Taratibu na sheria zilizopo sasa zirekebishwe ili kusaidia wanawake kuingizwa na kushirikishwa katika mkondo mzima wa uchumi.

### 3.4 Haki ya Kupata Elimu

Elimu ni mhimiri mmojawapo wa haki ya binadamu kama ilivyotajwa katika Tamko la Dunia la Haki za Binadamu (1949) na kuutambua uanuai kama sifa kuu ya binadamu. Uanuai huo hauna budi kutumika kama wenzo muhimu katika ujenzi wa jamii na taifa. Tanzania imeingia mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Haki za Mtoto (1989), ambao unabainisha haki ya kupata elimu na mafunzo hadi kufikia kiwango cha elimu ya juu cha kujitegemea na kuchangamana na jamii kwa kadiri inavyowezekana (UNESCO, 2005). Katika mazingira ya Tanzania, elimu inaweza

kufasiliwa kama mchakato unaochukua msimamo wa kimabadiliko katika kuandaa sera, shughuli na utamaduni ambao hujenga mazingira ya kielimu ambamo vikwazo vya uwepo, ushirikishwaji na ujifunzaji vinaweza kupunguzwa sana.

Elimu ni ufunguo wa maisha, ambapo, ukijenga mtandao wenye msingi imara na mzuri wa elimu, unazalisha wataalamu na nyenzo muhimu katika kupanga na kusimamia mipango ya maendeleo. Sekta hii ni pana, inahitaji fedha nyingi, majengo, madawati, vitabu vya kiada na ziada, walimu wenye ujuzi, maabara za kisasa, maslahi bora na nyumba bora za kuishi walimu. Serikali isipotenga fedha za kutosha kuhudumia elimu, itabaki kutoa ahadi zisizotekelezeka jambo ambalo ni hatari kwa ustawi na ufanisi katika kila sekta ya maendeleo hapa nchini na watu wake. Suala la ukosefu wa elimu lina madhara makubwa katika maendeleo ya jamii za ulimwengu. Baadhi ya jamii hazina kipaumbele kuhusu haki ya elimu kwa mwanamke kutokana na kuimarika kwa fikra potofu. Mwandishi anaeleza:

> Kama wazazi wake walivyokuwa, Siti hakupata kuona chuo chochote katika utoto wake. Kitabu kilikuwa kama gamba gumu sana hata katika utu uzima wake, alipokuwa amezungukwa na fahari (Uk. 6).

Maelezo haya yanaonesha umaskini na ujinga waliokuwa nao wazazi wa Siti ulisababisha kutokuwepo kwa kipaumbele katika suala la binti yao kupata elimu. Siti hakugusa hata chembe ya elimu. Matokeo yake, Siti alikosa fursa ya kurithi mali, kujikomboa kifikra, kiutamaduni na kuwa nyuma katika maendeleo ya kiuchumi, kiutamaduni na kisiasa. Elimu ni urithi pekee ambao hauwezi kulinganishwa na urithi wa vitu vingine kama vile pesa, mifugo, mashamba na rasilimali nyinginezo. Jitihada za makusudi zinapaswa kuchukuliwa zinazolenga kujenga misingi bora na imara ya kitaifa inayonuia kuimarisha elimu. Maendeleo ya sayansi na teknolojia katika nchi za viwanda yametokana na uwekezaji mkubwa katika elimu na elimu. Elimu inatazamwa kama kiini pekee cha maendeleo ya nchi kinachoiwezesha kukabiliana na mageuzi makubwa ya kisiasa na kiuchumi. Elimu ndicho chombo pekee kitakachoisaidia jamii kupata maarifa ya kutosha katika stadi zote za maisha.

Kama ilivyokuwa kwa Siti binti Saad kukosa elimu, hali na uzoefu unaonesha kuwa, watoto wa kike hawapewi kipaumbele kutokana na baadhi ya familia katika jamii za Kiafrika kutokana na kuwepo kwa mielekeo tofauti. Baadhi yake inamtazama mtoto wa kike kama hawezi kumudu harakati za kielimu, na kwamba, hana mchango katika ngazi ya familia yake kwa sababu ataolewa na kuungana na familia ya mumewe. Jamii haina budi kuondoa dhana potofu inayomtazama mtoto wa kike kama hastahiri kupata elimu. Ujenzi wa familia na taifa unahitaji ushirikiano thabiti kati ya wanawake na wanaume. Elimu haina budi kuwaongezea watu uhuru wao wa kimwili na kifikra; na kuweza kujiongoza wenyewe katika maisha na mazingira wanamoishi (Shule, 2004). Suala la umuhimu wa kusoma ili kujielimisha zaidi kwa manufaa ya

jamii na taifa ni la msingi kwa kila mwananchi. Umuhimu huo unatokana na ukweli kuwa elimu katika mataifa yanayoendelea haina budi kuwekewa misingi imara ili kumudu harakati za ustawi wa taifa na maendeleo yake.

Suala la ukosefu wa elimu ndilo linalowafanya wasichana wengi, hasa wanaotoka vijijini kuwa wategemezi na kujihusisha za kazi za uyaya katika miji na majiji hapa nchini. Pia, Baadhi yao wanaishia kuwa mama wa nyumbani kutokana na kuwepo kwa imani potofu kuwa mwanamke akijishughulisha na shughuli za uzalishaji mali kama vile biashara ndogo ndogo na ujasiriamali atasahau majukumu yake ya nyumbani ya uzazi na ulezi wa watoto. Hali hiyo humfanya kuchorwa kama mlezi wa familia na chombo cha starehe cha mwanaume kama mwandishi anavyoeleza:

> Siti binti Saad alionekana kama msaidizi katika maskani madogo ya wazazi wake masikini (Uk. 7).

Nukuu hiyo inaonesha namna mwanamkeanavyonyimwa haki ya kujishughulisha na shughuli nyingine za ujasiriamali kama vile biashara ndogo ndogo zinazoweza kumwingizia kipato ili kuzimudu changamoto za maisha katika mazingira yake. Matokeo yake ni kushindwa kusimama imara katika kila fani ya maendeleo katika jamii. Kushindwa kushiriki kikamilifu katika shughuli za kibiashara, hasa za uzalishaji mali na uchumi kunachangia kuporomoka kwa uchumi katika ngazi za familia na taifa kwa jumla (Kajeza, 2016). Wanawake lazima wasimame kidete kwa nguvu zao ili wajitetee na kupambana kwa dhati kwa sauti zao wenyewe na kuacha kuwategemea wanaume ambao kimsingi ndiyo wanaodhulumu haki wanazopigania. Wanawake hawana budi kupigania haki zao katika taifa lao ili kuhakikisha kuwa elimu, kazi, afya na huduma za kiuchumi zinatolewa kwa usawa. Kupigania haki zao ni pamoja na kuhakikisha kuwa wanawake wanashiriki katika nafasi mbalimbali za uongozi katika maeneo ya ngazi za maamuzi pasipo kubaguliwa.

## 4.0 Hitimisho

Katika makala hii sura ya mwanamke imeelezwa kwa namna mbalimbali katika riwaya teule. Jambo la kuzingatia ni kuwa jamii haina budi kupinga mambo yote yanayomdunisha mwanamke katika hali mbalimbali. Jamii haina budi kubadilika kulingana na mahitaji ya wakati kwani suala la umoja na mshikamano kati ya mwanamke na mwanaume ni la msingi katika ujenzi wa jamii na taifa. Jamii haina budi kupinga mtazamo hasi dhidi ya mwanamke kupitia harakati za serikali na taasisi zisizo za kiserikali ili kupinga na kukemea hali yoyote inayonuia kumtazama mwanamke katika mtazamo hasi zitawasaidia wanawake kufanikisha wajibu wao katika jamii. Umoja ni fimbo ya mnyonge katika jamii na taifa lolote. Mwanamke hana budi kutazamwa katika mtazamo chanya kwa sababu ni mhimiri imara katika ujenzi na harakati za maendeleo ya jamii na taifa.

**Marejeleo**

Bond, S. (2000). 'Culture and Feminine Leadership', *In Women Power and the Academic From Rhetoric to Reality*. New York: Berghahn Books.

Challigha, N. E. (2011). Usawiri wa Mwanamke na Mgawanyo wa Majukumu Kijinsia katika Fasihi Picha ya Katuni Mnato za Kiswahili. Tasinifu ya Uzamili (Haijachapishwa).Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Fakih, S. (2017). Kutathimini Mabadiliko ya Usawiri wa Mwanamke katika Riwaya ya *Utengano* na *Kamwe si Mbali Tena*: Utafiti Linganishi. Tasinifu ya Uzamili (Haijachapishwa).Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Githuci. M. C. (2013). *Ujagina wa mwanamke katika Pango.*Tasinifu ya Shahada ya Uzamili (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Nairobi.

Kajeza, R. T. (2016). Usawiri wa Mwanamke katika Fasihi Andishi: Mifano Kutoka katika riwaya ya *Machozi na Damu* ya E. Shigongo (2005). Tasinifu ya Shahada ya Kwanza (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Tumaini Makumira.

Khatibu, M. S. (2011). *Chanjo, Matakwa ya Mwanaume Katika Mwili wa Mwanamke: Ulinganisho wa Ushairi wa Muyaka na Shaaban Robert.* Dar es Salaam: Taaluma ya Taasisi za Kiswahili.

Kitundu, N, J. (2012). Usawiri wa Wahusika Wanawake Katika Ngano za Kinyiramba. Tasinifu ya Shahada ya Uzamili (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Lyatuu, J. (2011). Usawiri wa Wanawake katika Fasihi ya Kiswahili: Ulinganifu wa Waandishi wa Kike na Kiume: Uchaguzi katika Riwaya Teule. Tasinifu ya Uzamili (Haijachapishwa).Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Mabuba, B. P. (2015). *Akupendaye Mpende: Sonata za Shakespeare*. Dodoma: Publications.

Maganga, M. (2015). Usawiri wa Mwanamke katika Riwaya ya *Pesa Zako Zinanuka*. Tasinifu ya Shahada ya kwanza (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Tumain Makumira.

Mapunjo, G. C. (2014). Usawiri wa Mwanamke Kama Kiongozi Katika Tamthiliya: Uchunguzi wa Kivuli Kinaishi na Nguzo Mama. Tasinifu ya Uzamili (HAijachapishwa). Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Massoud, H. S. (2018). Kutathimini Usawiri wa Mwanamke katika Riwaya ya Mfadhili. Tasinifu ya Uzamili (Haijachapishwa).Chuo Kikuu Huria Cha Tanzania.

Mbiu, C. (2013). Usawiri wa Mwanamke katika Ngano za Kisambaa. Tasinifu ya Uzamili

(Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Mugane, D. (2012). Nafasi ya Mwanamke katika Jamii. USA: Harvard Univesity Press.

Omary, S. (2009). Tanzanian Hip Hop Poetry a Popular Literature. Tasinifu ya Uzamivu (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Oyeronke, O. (2005). *African Gender Studies*. New York: Palgrave MacMillan.

Pullen, C. (2006). *Marxist Against Feminists on Education*. London: Routledge.

Robert, S. (1991). *Wasifu wa Siti Binti Saad*. Dar es Salaam: Mkuki na Nyota Publishers.

Ruto, M. C. (2015). Matatizo ya Mwanamke katika Kidagaa Kimemwozea na Nyuso za Mwanamke. Tasnifu ya Uzamili (Haijachapishwa).Chuo Kikuu cha Nairobi.

Sanga, A. (2013). 'Wanawake na Injili katika Ujasiriamali'. Dar es Salaam: Ujuzi Education Publishers Limited.

Shule, V. (2004).'Effective Video Film Reducing Young Womens Gender Violence and Other. HIV Risk Behaviours'. A Research for Master Degree (Unpublished). University of Dar es Salaam.

Sungi, N. A. (2011). Ruwaza ya Shujaa Mwanamke wa Kiutendi katika Jamii ya Wanyanyembe wa Tabora. Tasinifu ya Uzamili (Haijachapishwa).Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

UN (2014).*Gender Equality and Sustainable Development.* The Data Section of UN Women, United States: AGS Custom Graphics, RR Donnelly Company.

UNESCO, (2005). 'Guidelines for Inclusive Education Policy Development. Working Towards Education for All'. Harare: UNESCO.